JINA: …….NAMBARI YAKO: ……

DARASA……..……..…SAHIHI……TAREHE:……

102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA 3
Saa: 2½
2019

Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari
MJJARABU WA KWANZA
Karatasi ya tatu
Saa: 2½

<u>Maagizo</u>:
(a) Jibu maswali **manne** pekee
b). Swali la **kwanza** ni ya **lazima**
c). Maswali hayo mengine matatu kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Riwaya, Hadithi Fupi,ushairi na fasihi simulizi
d). Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja
e). Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Karatasi hii ina kurasa 6 zilizochapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hizi zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU YA A: (LAZIMA) TAMTHILIA- KIGOGO (*Pauline Kea*)

1. "…huoni kisima kimeingiwa paka na maji hayanyweki tena?"

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
b) Eleza sifa zozote nne za msemaji wa maneno haya (alama 4)
c) Fafanua umuhimu mbili za mzungumzaji (alama 2)
d) Taja mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa katik dondoo (alama 2)
e) Thibitisha ukweli wa kauli kuwa 'kisima kimeingiwa paka na maji hanyweki tena' ukirejelea tamthilia ya kigogo (alama 8)

SEHEMU A B: RIWAYA- CHOZI LA HERI *(Assumpta K. Matei)*

Jibu swali la 2 au la 3

2. "Unajua kwamba mimi sikuumbiwa ujaalana, walimwengu ndio walionifinyanga upya, wakanipa moyo wa ujabari."

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
b) Fafanua sifa zozote mbili za mzungumzaji (alama 2)
c) Mzungumzaji ana umuhimu gani katika riwaya? (alama 2)
d) Fafanua kilichomsababisha mzungumzaji kuwa na moyo wa ujubari (alama 2)
e) Taja tamathali zozote mbili zilizotumika katika dondoo (alama 2)
f) Eleza jinsi maudhi ya ujaala ulivyojitokeza kwenye riwaya (alama 12)

Au

3. Ukiukaji wa haki za kibinadamu ni jambo la kawaida katika baadhi ya nchi zinazoendelea. Kwa kurejela riwaya ya Chozi la Heri, thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

SEHEMU YA C: HADITHI FUPI- TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

(Dumu Kayanda na Alifa Chokocho)

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Mimi tangu hapo najijua bwana. Sina moyo wa bua."

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
b) Taja tamathali ya usemi iliyotumiwa katika dondoo (alama 2)
c) Kauli hii ni kinaya. Fafanua kwa mujibu wa hadithi (alama 4)
d) Fafanua changamoto ambazo wazazi pamoja na vijana hupitia kwa kurejelea hadithi (alama 10)

Au

5. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine, jadili namna ambavyo wahusika wa kike wamesawiriwa (alama 20)

SEHEMU YA D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7

6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ewe

Ndiyo, ewe upitaye majiani

Kwa maringo na kwingi kujishasha

Unayenitazama kwa chuki kwa sababu

Ya mavazi yangu

Mavazi yaliyochakaa

Mavazi yaliyofukaa

Mavazi ya kiufukara

Ewe

Ndiyo, ewe unionaye kama tauni

Unionaye na kutimua mbio kwa hofu

Unionaye na kupiga mkubwa usiahi

Kwa ajili ya sura yangu

Sura yangu iliyoharibika

Sura yangu iliyobadilika

Sura yangu ya kimaskini.

Ewe

Ndiyo, ewe uniashiriaye kwa mbali

Kunionyesha kama mnyama mbuani

Unayeogopa kunikaribia

Ukayaona jinsi ninavyoishi

Jinsi ninavyoishi maisha yangu

Maisha yangu ya kusikitisha

Maisha yangu yanayotisha

Maisha ya kifakiri.

Umefanya nini?

Umesema nini?

Niache maisha duni

Uniitaye mtoto wa mitaani.

Maswali

a) Tambua shida zozote tano zinazomkumba mzungumzaji (alama 5)
b) Ainisha shairi hili kisha utoe sababu (alama 2)
c) Tambua tamathali za usemi zilizotumika kwenye shairi hili (alama 3)
d) Eleza umuhimu wa aina mbili za urudiaji zilizotumika katika shairi (alama 4)
e) Tambua mshata katika shairi hili (alama 1)
f) Eleza jinsi malenga alivyotumia kibali chake (alama 1)
g) Tambua nafsi neni katika shairi hili (alama 1)
h) Eleza muundo wa shairi hili (alama 1)

Au

7. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Mkata ni mkatika, haridhi hatoridhiwa

Sina ninalilishika, wala ninalochukuwa

Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!

Mrithi nini wanangu?

Sina ng’ombe sina mbuzi, sina konde sina buwa

Sina hata makaazi, mupasavyo kuyajuwa

Sina mazuri makuzi, jinsi nilivyoachwa

Mrithi nini wanangu?

Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa

Sina chembe ya majazi, mno ni kukamuliwa

Nakwa’cheni upagazi, ngumu kwenu ku’tuwa

Mrithi nini wanangu?

Sina sikuachi jina, mkata hatasifiwa

Hata nifanye la mana, mno mi kalaumiwa

Poleni wanangu sana, sana kwenu cha kutowa

Mrithi nini wanangu?

Sina leo sina jana, sina kesho kutwaliwa

Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa

Sina wanangu mi sina, sana la kuacha kuraduwa

Mrithi nini wanangu?

Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa

Nyuma yangu ili dhiki, na mbele imekaliwa

N’nawana na milki, hadi nitakapofukiwa

Mrithi nini wanangu?

Sina ila kesho kwenu, wenyewe kuiongowa

Muwane kwa nyingi mbinu, mwende pasi kupumuwa

Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa

Mrithi nini wanangu?

Maswali

a) Taja mambo yoyote mawili ambayo mtunzi angewarithisha wanawe (alama 2)
b) Eleza sababu ya mtunzi kutoweza kuwarithisha wanawe (alama 2)
c) Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari alama 4)
d) Dondoa mifano miwili ya (alama 2)
    i) Inkisari
    ii) Tabdila

e) Chambua shairi hili kwa upande wa

    i) Dhamira

    ii) Muundo

f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumiwa katika shairi (alama 3)

    i) Mlimwengu kanipoka

    ii) Sina konde sina buwa

    iii) Wingi wa shakawa

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8) a) Fafanua umuhimu wa fomyula ya kumalizia katika hadithi (alama 5)

b) Bainisha vipera vyovyote btatu vya hadithi (alama 3)

c) Methali ni utanzu tegemezi. Fafanua (alama 5)

d) Misimu ni nini? (alama 2)

e) Fafanua umuhimu wa misimu katika jamii (alama 5)